



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA



TANGAZO

TANGAZO

TANGAZO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA ANAWATANGAZIA WAFUGAJI WOTE NA WADAU WA SEKTA YA MIFUGO KWAMA KUTAKUWA NA ZOEZI LA CHANJO YA MIFUGO KITAIFA KUENZIA TAREHE 25/01/2025 KWA NG'OMBE, MBUZI, KONDOO NA KUKU.

LENGO NI KUDHIBITI VIFO VYA MIFUGO, KUBORESHA AFYA YA MIFUGO NA KUONGEZA UZALISHAJI.

CHANJO ITAKUWA DHIDI YA UGONJWA WA HOMA YA MAPAFU KWA NG'OMBE, SOTOKA KWA MBUZI NA KONDOO NA KIDERI (UBABA) KWA KUKU


GHARAMA ZA UCHANJAJI NI KAMA IFUATAVYO;

- HOMA YA MAPAFU KWA KUCHANGIA TSH 500/= TU KWA KILA NG'OMBE.
- SOTOKA YA MBUZI NA KONDOO KWA KUCHANGIA TSH 300/= TU KWA KILA MBUZI AU KONDOO
- KIDERI (UBABA) KWA KUKU AMBAYO ITATOLEWA BURE.

GHARAMA ZA UCHANJAJI ZIMESHUKA KWA SABABU SERIKALI INAYONGOZWA NA MHE RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA Dr. SAMIA SULUHU HASSAN IMETOA RUZUKU YA CHANJO NA KUPUNGUZA GHARAMA KWA ASILIMIA HAMSINI (50%).

HIVYO WAFUGAJI WOTE MNAOMBWA KUUNGA MKONO JUHUDI ZA SERIKALI YETU KWA KUJITokeza kwa wingi na kupeleka mifugo kwenye maeneo ya kuchanja katika siku mtakayo pangiwa kwenye vijiji vyenu. RATIBA KAMILI YA CHANJO KWA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA ITATOLEWA MAPEMA BAADA YA KUKAMILIKA KWA MAANDALIZI YA ZOEZI HILI.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 13/01/2025.


Maisha S. Mtipa
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA.

Nakala: Mbao zote za matangazo.